# WIKI YA MAOMBI KWA UMOJA WA WAKRISTO

*na kwa mwaka mzima*

2024

Mpende Bwana Mungu wako… na jirani yako kama nafsi yako

Luka 10:27

# YALIYOMO

DIBAJI NA MWENYEKITI...............................................................................................1

Kwa wanaoandaa Wiki ya Maombi kwa Umoja wa Wakristo ..........................................................2

Nakala ya Biblia kwa mwaka 2024...........................................................................................3

Utangulizi wa mandhari ya mwaka 2024.....................................................................................4

Ibada ya Kiekumene
Maelekezo kwa waandalizi wa ibada.........................................................................................7
Utaratibu wa ibada ....................................................................................................................8

Tafakari za kibiblia na Maombi ya Siku Nane ..........................................................................15

Kiambatisho 1: Nyimbo zinazopendekezwa kwa ibada ..........................................................26
Kiambatisho 2: Sala kwa Umoja wa Wakristo kufuatana na Jamii ya *Chemin Neuf*........................29
Kiambatisho 3: Ofisi ya Umoja wa Wakristo kufuatana na Jamii ya *Chemin Neuf* .........................30

IEM –K.........................................................................................................32

Dondoo za kibiblia: Dondoo za kibiblia katika kijitabu hiki zimetolewa katika The New Revised Standard Version ya Biblia Takatifu haki ya kunakili © 1989, 1995 na Kitengo cha Elimu ya Kikristo cha Baraza Kuu la Makanisa ya Amerika na yanatumika kwa idhini ya wachapishaji. Haki zote zimehifadhiwa

## KWA WANAOANDAA

# WIKI YA MAOMBI KWA UMOJA WA WAKRISTO

## Utafutaji wa Umoja kwa Mwaka Mzima

Kipindi cha jadi cha Wiki ya Maombi kwa Umoja wa Wakristo katika ulimwengu wa kaskazini ni Januari 18-25. Tarehe hizo zilipendekezwa mwaka 1908 na Paul Watson zikilenga msimu kati ya sikukuu ya Mtakatifu Petero na ya Mtakatifu Paulo, na kwa hivyo zina maana ya kiishara. Katika ulimwengu wa kusini ambako wakati huu ni wa mapumziko, makanisa kwa kawaida hutafuta siku nyingine za kusherehekea Wiki ya Maombi, kwa mfano wakati wa Pentekoste (ilivyo pendekezwa na harakati ya Imani na Utaratibu mwaka 1926), kwa vile wakati huu pia unaashiria umoja wa makanisa.

Ili kuwezesha kila mtu kutumia kijitabu hiki kwa wakati wake, tunawaalika kukitumia mwaka mzima ili kuonyesha umoja wa makanisa ambao makanisa yamefika, na kuombea umoja kamili alivyotamani Yesu Kristo.

## Urekebishaji wa maandishi

Inatumainiwa kwamba kadiri inavyowezekana, kijitabu hiki kitarekebishwa kulingana na matakwa ya watakaokitumia. Ni muhimu kutilia maanani liturjia ya wenyeji na mazoea yao ya ibada pamoja na muktadha wa kijamii na kitamaduni.

Ni muhimu kutilia maanani desturi za kiliturjia na ibada ya wenyeji pamoja na muktadha wa kijamii na kitamaduni. Ni bora kufanya hayo marekebisho kiekumene. Katika maeneo kadhaa, tayari kuna mbinu za kiekumene za kurekebisha naandishi.

## Jinsi ya kutumia yaliyomo wakati wa Wiki ya Maombi

Kwa makanisa na jumuiya za Kikristo zinazo sherehekea Wiki ya Maombi pamoja katika ibada, kuna Utaratibu wa Maombi ya kiekumene. Makanisa na jumuiya za Kikristo wanaweza pia kutumia kijitabu hiki katika ibada zao wakati wa Wiki ya Maombi. Maombi kutokana na ibada ya kiekumene, "Siku Nane", na baadhi ya sala zilizochaguliwa pia zaweza kutumika inavyofaa kulingana na mazingira.

Jumuiya zinazofuata ratiba ya Wiki ya Maombi kila siku zaweza kutumia maombi yalivyo kwenye ratiba ya "Siku Nane".

Wale wangependa kufuatilia masomo ya Biblia kwa kutumia maudhui ya Wiki ya Maombi wanaweza kutumia maandishi na tafakari za "Siku Nane". Majadiliano ya kila siku mwaka huu ikiwemo changamoto yaweza kukamilika kwa maombi ya maombezi.

Wale wangependa kuomba faraghani watanufaika na yaliyomo wakilenga nia zao ingawa inafaa wakumbuke kuwa wako pamoja na wengine wakiombea umoja wa Kanisa la Kristo ulimwenguni kote.

# NENO LA BIBLIA KWA MWAKA 2024

Luka 10:25-37
Neno: Bibilia Takatifu

25 Mwalimu mmoja wa sheria alisimama akajaribu kumpima Yesu, akamwuliza, “Mwalimu, nifanye nini
ili nipate uzima wa milele?” 26 Yesu akamjibu, “Sheria inasemaje? Unaitafsiri vipi?” 27 Yule mwalimu
wa sheria akajibu, “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa
nguvu zako zote na kwa akili zako zote. Na umpende jirani yako kama unavyojipenda
mwenyewe.” 28 Yesu akamwambia, “Jibu lako ni sahihi. Fanya hivyo nawe utaishi.” 29 Lakini yule
mwalimu wa sheria akitaka kuonyesha kwamba hoja yake ilikuwa na maana zaidi, akamwuliza Yesu,
“Na jirani yangu ni nani?”
30 Yesu akamjibu, “Mtu mmoja aliteremka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. Njiani akashambuliwa
na majambazi; wakamwibia kila kitu alichokuwa nacho, wakampiga wakamwacha karibu ya
kufa. 31 Ilitokea kwamba kuhani mmoja alikuwa anapitia njia ile. Alipomwona huyo mtu, akapita
upande mwingine wa barabara akamwacha hapo hapo. 32 Vivyo hivyo Mlawi mmoja naye alipopita,
alimwona, akapita upande mwingine wa barabara akamwacha hapo hapo.
33 “Lakini Msamaria mmoja aliyekuwa akisafiri kupitia njia hiyo alipomkuta, alimwonea
huruma, 34 akamwendea akasafisha majeraha yake kwa divai na mafuta, akayafunga. Kisha akamweka
kwenye punda wake akaenda naye mpaka nyumba ya wageni ambapo alimtunza. 35 Kesho yake, yule
Msamaria alipokuwa anaondoka, akampa mwenye nyumba ya wageni fedha akamwomba amtunze
yule mgonjwa na akaahidi kulipa gharama yoyote ya ziada atakaporudi.
36 “Unadhani ni yupi kati ya hawa watatu alikuwa jirani yake yule mtu aliyeshambuliwa na majambazi?”
37 Yule mwalimu wa sheria akajibu, “Ni yule aliyemwonea huruma.” Yesu akasema, “Nenda ukafanye
vivyo hivyo.”

**Neno: Bibilia Takatifu (SNT)**
Haki ya kunakili © 1989 na Biblica

# UTANGULIZI WA MAUDHUI
# YA MWAKA 2024

Mpende Bwana Mungu wako… na jirani yako kama nafsi yako
Luka 10:27

Maandishi ya Wiki ya Maombi ya mwaka 2024 yalitayarishwa na kikundi cha kiekumene nchini Burkina Faso wakisaidiwa na jumuiya ya *Chemin Neuf* (CCN).[1] Maudhui waliochagua ni "Mpende Bwana Mungu wako… na jirani yako kama nafsi yako. (Luka 10:27)

Waumini kutoka Jimbo Katoliki la Ouagadougou, makanisa ya Kiprotestanti, vikundi vya kiekumene, pamoja na CCN Burkina Faso walishirikiana kwa ukarimu kwa minajili ya kutayarisha maombi na tafakari na wakaona kazi yao pamoja kama njia kamili ya uongofu wa kiekumene.

## Kumpenda Mungu na jirani wakati wa mgogoro wa kiusalama

Burkina Faso imo Afrika Magharibi kwenye eneo la Sahel, inayojumuisha nchi jirani za Mali na Niger. Ina upeo wa kilomita 174,000 mraba na idadi wa watu milioni 21, kutoka makabila sitini hivi. Kidini, asilimia 64 ya watu ni Waislamu, asilimia tisa ni wa dini za jadi za Kiafrika na asilimia 26 ni Waskristo (Wakatoliki asilimia 20, and Waprotestanti asilimia sita). Dini hizi tatu zimepenya kila jimbo nchini na kila familia.

Kwa wakati huu, Burkina Faso imekumbwa na mgogoro wa kiusalama unaoathiri mashirika yote ya kidini. Tangu shambulio la kijihadi la mwaka 2016, hali ya usalama nchini Burkina Faso imezidi kuzorota pamoja na utangamano wa kijamii. Mashambulizi ya kigaidi yameenea nchini kote pamoja na uasi-sheria na biashara ya binadamu. Kadiri ya watu elfu tatu wamepoteza maisha hali karibu milioni mbili wengine hawana makao nchini mwao. Maelfu ya shule, vituo vya afya na kumbi za starehe mijini zimefungua. Miundo misingi ya Starehe, uchumi na hata usafiri imeharibiwa. Mashambulizi dhidi ya makabila fulani yamechochea hatari ya migogoro baina ya jamii. Kutokana na haya yote, hali ya usalama nchini, utangamano wa kijamii, amani na umoja wa kitaifa imezidi kudhoofika.

Makanisa yamelengwa kwa mashambulizi. Mapadre, wachungaji na wakatekista wameuawa nyakati za ibada na hali ya waliotekwa nyara haijulikani. Tunapoandika ripoti hii, zaidi ya asilimia 22 ya nchi iko nje ya mamlaka ya serikali. Wakristo hawawezi kuabudu hadharani. Kwa sababu ya ugaidi, wingi wa makanisa kaskazini, mashariki na kaskazini-magharibi ya nchi yamefungwa. Kwa sasa hakuna ibada za Kikristo hadharani kwenye wingi wa maeneo haya. Kunako ibada chini ya ulinzi wa polisi, sana sana majijini, imebidi hizo ibada zifupishwe kutokana na hofu za kiusalama.

Inabidi ieleweke kwamba licha ya jitihada za serikali na jumuiya za kidini, nchi imeendelea kupoteza utulivu kadiri makundi yenye misimamo mikali yanavyo enea nchini. Hata hivyo, kuna dalili ya kuchipuka kwa ushikamano kati ya Wakristo, Waislamu na wafuasi wa dini za jadi. Vyongozi wao wanashughulikia kupata suluhisho la kudumu kwa minajili ya amani, utangamano wa kijamii, na upatanisho. Kwa mfano, Tume ya Mazungumzo ya Wakristo na Waislamu chini ya Baraza la Maaskofu wa Kikatoliki wa Burkina Faso limejitahidi kuunga mkono mazungumzo yanayolenga ushirika kati ya dini na makabila tofauti.

Kufuatia wito wa serikali kuombea amani, utangamano wa kijamii, na upatanisho, baadhi ya makanisa yanaendelea kuandaa maombi ya kila siku na kufunga. Makanisa kadhaa ya Kikatoliki na Kiprotestanti yametilia mkazo jitihada za kuwasaidia watu waliohamishwa makwao. Mikutano ya kutafakari na kuongeza ufahamu imeandaliwa kukuza ufahamu zaidi kuhusu hali ya nchi na thamani ya undugu na kukuza mbinu za kuleta amani ya kudumu. Tumaini hili pia lajionyesha kwa msemo wa Wamossi[2]: "Licha ya hali na urefu wa mapigano, wakati wa mapatanisho utafika."

Mwaliko wa kushirikiana kwa minajili ya kutayarisha masomo ya Wiki la Maombi ya Umoja wa Wakristo 2022 unayapa changamoto makanisa mbalimbali ya Burkina Faso kutembea, kuomba na kufanya kazi pamoja kwa upendo wakati huu mgumu nchini kwao. Upendo wa Kristo unaounganisha Wakristo wote una nguvu kuliko migawanyiko yao na Wakristo wa Burkina Faso wanajitolea kutembea katika upendo wa Mungu na upendo wa jirani. Wana imani kwamba upendo wa Mungu utashinda vurugu inayokumba nchi yao.

## Somo la kibiblia

**Umuhimu wa upendo katika maisha ya Kikristo**

Upendo ndio 'DNA' ya imani ya Kikristo. Mungu ni upendo na "upendo wa Kristo umetukusanya kuwa kitu kimoja".[3] Utambulisho wetu wa pamoja unatokana na uzoefu wetu wa upendo wa Mungu (linganisha na Yohana 3:16) na huonyesha utambulisho huo ulimwenguni kote kulingana na vile tunavyopendana. (Yohana 13:35) Katika kifungu kilichoteuliwa kwa minajili ya Wiki ya Maombi kwa Umoja wa Wakristo 2024 (Luka 10:25-37), Yesu alisisitiza mafunzo ya Kiyahudi kutokana na Kumbukumbu ya Torati 6:5: "Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote, na kwa akili yako yote… Na (Walawi 19:18b), "mpende jirani yako kama nafsi yako."

Kisha mwanasheria katika kifungu cha injili anamuuliza Yesu, "na nani jirani yangu?" Swali kuhusu kimo cha upendo kibiblia mara nyingi lilizusha ubishi miongoni mwa wasomi wa sheria. Kijadi, jukumu hili liliaminiwa kuhusu tu Waisraeli wenza na wageni wakazi wa Israeli. Baadaye, kutokana na uvamizi wa kigeni, amri ikaanza kueleweka kama vile haikuhusu wageni kutoka vikosi vya wavamizi wa kukalia. Na vile Uyahudi ulivyogawanyika, amri kwa wakati mwingine ilianza kueleweka kama ilihusu tu kikundi cha mtu. Kwa hivyo, swali aliloulizwa Kristo lilikuwa la uchochezi. Yesu alijibu kwa kusimulia mfano wa upendo wenye upeo uliozidi alivyotarajia mwanasheria huyo.

Waandishi wa Kikristo wa hapo kale kama vile Orijeni, Klementi wa Alexandria, Yohana Krisostom na Agustino waliona njia na mpango wa Mungu kwa wokovu wa ulimwengu katika mfano huu aliosimulia Kristo. Waliona mtu aliyekuwa akienda Yerusalemu kama mfano wa Adamu – yaani wanadamu wote – wakitoka paradiso kuja duniani, panapo hatari nyingi na kuvunjika roho, na wanyang'anyi wakiwa mfano wa ulimwengu wenye nguvu za uadui zinazotukumba. Walimuona Kristo kama alieyeshikwa na huruma, akija kumusaidia msafiri aliyekuwa hali mahututi., akamtibu vidonda na kumpeleka kwa usalama wa nyumba ya wageni, ambayo wasomi wa Kikristo waliona kama mfano wa kanisa. Ahadi ya Msamaria kurudi ilichukuliwa kama ishara ya ahadi ya Kristo kurudi tena.

1. Wamossi ndio kabila kubwa Zaidi nchini Burkina Faso.
2. *Ubi caritas* (inahusishwa na Paulinus wa Akuileya).

Wakristo wanaitwa kutenda kama Kristo kwa kupenda kama Msamaria Mwema, wakionyesha neema na huruma kwa wale walio na mahitaji bila kujali dini, kabila na hali yao ya kijamii. Hatupaswi kushinikizwa tu na utambulisho wa pamoja kusaidia wengine, ila upendo wa 'jirani'. Hata hivyo, maono ya upendo kwa jirani tunao onyeshwa na Kristo yamekumbwa na mambo mengi.

Uwezo wetu wa kupenda kama vile Kristo anatupenda unakabiliwa na mapigano kwenye majimbo mengi, ukosefu wa usawa katita uhusiano wa kimataifa na unaletwa na mipango ya marekebisho ya miundo na nchi za magharibi au mashirika ya nje. Kujifunza kupendana bila kujali tofuti zetu ndio utatufanya majirani kama Msamaria anayesumuliwa takika Biblia.

## Njia ya Uekumene

Yesu aliomba kwamba wafwasi wake wote wawe kitu kimoja. (Fananisha na Yohana 17:21), na kwa hivyo, Wakristo hawawezi kufa moyo wala kuacha kuomba na kufanya kazi ya kuleta umoja. Wako pamoja katika upendo wao wa Mungu katika Kristo na jinsi wanavyoelewa upendo wa Mungu kwao. Wanatambua hii kutokana na imani yao baina yao wanapo omba, kuabudu na kumtumikia Mungu pamoja. Hata hivyo, katika uhusiano wa kimakanisa, ya Burkina Faso ikiwemo, hali hii bado inazusha changamoto. Hali ya makanisa kutojuana, na shuku miongoni mwao, inaweza kudhoofisha kujitolea kiekumene. Baadhi ya Wakristo huenda wakahofia kupoteza utambulisho wao wa kimadhehebu na kuzuia kanisa lao 'kukuwa'. Mabishano ya aina hiyo kati ya makanisa ni kinyume na ombi la Kristo. Kama kuhani na Mlawi katika kifungu cha injili. Mara nyingi Wakristo hupoteza nafasi ya kuungana na kaka na dada zao kwa sababu ya uoga. Wakati wa Wiki la Maombi kwa Umoja wa Wakristo, tunaomba Bwana yetu aje kutusaidia, kutunza majeraha yetu na kutuwezesha kutembea kiekumene kwa kujiamini na matumaini.

## Umoja wa Wakristo kwa huduma ya amani na upatanisho

Hali kamili ya Burkina Faso yaonyesha haja ya kuweka upendo katikati ya utafutaji wa amani na upatanisho. Mara nyingi utafutaji huu umedhoofishwa na kupotea kwa maadili na ubinadamu wetu wa pamoja na kudhoofika kwa kujali manufaa ya wema wa pamoja, uadilifu na uzalendo. Utafutaji wa upatanisho pia umedhoofishwa na umaskini wa kiroho na kutafuta mali kwa njia rahisi. Dhidi ya ukweli huu, ni muhimu kushuhudia upendo wa Mungu zaidi.

## Kuacha migawanyiko na kuelekea umoja Burkina Faso

Jumuiya za Kikristo Burkina Faso zinajaribu kuishi kufuatana na wito wa upendo kupitia ukarimu. Hii ni wazi zaidi wakati wa Wiki ya Maombi kwa Umoja wa Wakristo. Wamejitolea kiutu na kifedha kutafsiri maandishi ya Biblia ya Kifaransa ya kiekumene (*Traduction Œcuménique de la Bible*) kwa lugha za kienyeji, hivyo wakisaidia kuongoza Wakristo hadi 'nyumba ya wageni' ya neno la Mungu (kwa mfano Lk 10:34). Zaidi ya hayo, wanatembeleana makanisani na kuabudu pamoja. Pia wanashirikiana kwa kuendeleza undugu, utu, amani na usalama nchini Burkina Faso. Wanapeleka Kristo kwa wenzao wanapotunza vidonda vya waliokumbwa na umaskini na maisha magumu.

Hata hivyo, kufuatana na msemo wa Kiafrika, "Kamwe mti usifiche pori". Mifano hii ya kiekumene haiwezi kuficha ukweli kwamba bado kuna changamoto nyingi dhidi ya umoja. Licha ya juhudi zao za kuwa jirani kwa wote wanaoamini Utatu wa Mungu, makanisa Burkina Faso hupambana kupendana kufuatia amri ya Kristo. Wakati mwingine wanahusiana kama Wasamaria na Wayahudi, wakiwa na migawanyiko ya kimila na kiteolojia na kuishi katika mazingira yasio urafiki na katika uhusiano wa chuki. Mfarakano unaondelea huwaharibu na kwa hivyo, wanatambua umuhimu wa mazungumzo ya kiekumene ili waweze kitia mafuta na mvinyo wa uponyaji kwa vidonda vya wenzao.

Nyumba ya wageni katika mfano wa Msamaria Mwema mara nyingi ulichukuliwa na Baba wa Kanisa kumaanisha kanisa. Vile Msamaria alivyompeleka msafiri aliyejeruhiwa kwenye nyumba ya wageni, vivyo hivyo Kristo anawakabithi majeruhi wa ulimwengu na wanaokosa mahitaji muhimu kwa makanisa kutunza hisia zao za kuvunjika na kuwasaidia kurudi katika hali ya afya. Utume huu unaohudumia ulimwengu wote ni ya njia moja ya kuleta amani ambayo ni zawadi ya Mungu kwa watu wake.

# IBADA YA KIEKUMENE

## *Maelezo kwa watayarishi wa ibada*

Mwaka huu ibada ya kiekumene ilitayarishwa na kikundi kilicho wakilisha madhehebu tofauti ya Kikristo nchini Burkina Faso wakisaidiwa na Jamii ya *Chemin Neuf* (CCN).

Masomo ya Biblia na liturjia yanatokana na mfano wa Msamaria Mwema ikiambatana na picha yake. (Luka 10: 25-37) Yesu anaonyesha maana ya kumpenda jirani akijibu swali lililotokana na swali aliloulizwa kutokana na amri ya Agano la Kale: "Mpende Bwana Mungu wako… na jirani yako kama nafsi yako." (Kumbukumbu ya Torati 6:5 na Walawi 19:18b).

Ili kujitayarisha kwa ibada, vifaa kadhaa zinahitajika. Kwa kitendo cha kukusanyika, chenye Kushiriki Upendo wa Mungu, kibuyu au chombo kilichojaa maji chahitajika. Ibada inaanza na msafara wa wasaidizi wakiwa na kibuyu au chombo kinachofaa wakielekea pahali patakatifu msomaji akialika jamii kukusanyika. Mmoja wa wenyeji anapeana maji kutoka kwa kibuyu kwa waakilishi wa jumuiya zingine waliopo kunywa maji hayo. Kitendo hiki chaweza pia kufanyika mlangoni mwa kanisa. Kitendo hiki cha makaribisho kinapokwisha, viongozi wa ibada na waakilishi wa jumuiya zilizopo wanajiunga na msafara, hivi wimbo au muziki ukichezwa.

Wakristo kutoka Afrika Magharibi wakiwepo kwenye sherehe, ni bora kuwaalika kuimba wimbo kwa lugha yao wakati wa ibada. Kadhalika, shada la maua yenye rangi tofauti laweza kuletwa mbele na waakilishi wa makanisa mbalimbali waliopo – kuonyesha wingi wa upendo wa Mungu na tofauti za watu wa Mungu.

Masomo ya kiongozi (K) yanaweza kugawanywa kati ya makasisi waliopo au waakilishi wa tamaduni mbalimbali zilizopo. Kadhalika, masomo ya msomaji (M) yanaweza kugawanywa kati ya watu toufauti waliopo.

Baada ya ibada, kibuyu au chombo cha maji kinaletwa mbele na kuinuliwa mbele ya waumini kiongozi anapotangaza mwisho wa ibada. Kutumwa na kubarikiwa kwaweza kutangazwa na makasisi au waakilishi wa jumuiya tofauti zilizopo.

# *Utaratibu wa Ibada*

K Kiongozi
M Msomaji
W Waumini

## Kukusanyika na Kushiriki Neno la Mungu

M Kibuyu nchini Burkina Faso hutumika kunywa maji na wageni wanapowasili hali wamechoka kwa safari. Ni ishara ya makaribisho, ukarimu na ushirika. Baada ya mgeni kuchangamka, mazungumzo yanaweza kuanza na sababu ya ugeni kutajwa. Tunapokusanyika na kuanza maombi, twawakaribisha jinsi Abrahamu alivyo wakaribisha wageni watatu akawapa maji kuwaburudisha. Twawakaribisha muburudike kwa kunywa maji ya kibuyu pamoja.

*Mmoja wa wenyeji anagawa maji ya kibuyu kwa waakilishi wa wamakanisa mbalimbali waliopo. Kibuyu kinaporudishwa pahali patakatifu, viongozi wa ibada wanajiunga na msafara wimbo au muziki ikichezwa.*

## Mwaliko wa Kuomba

K Kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu.
**W Amina.**

K Tuko hapa kama kaka na dada kuombea umoja wa Wakristo ulio wazi. Kiini cha ibada hii ni hadithi ya Msamaria Mwema tunaposikia wito wa kumpenda Mungu na kumpenda jirani kama nafsi yetu.

Hebu tujitayarishe kukutana na Mungu wa Upendo kwa shukrani na furaha, tukikumbuka amri yake ya kupendana.

**K Utukufu kwako, Baba, kwa maana wajifumbua kwa viumbe vyako na kuita watu wote waishi mbele yako.**
**Utukufu kwako, Kristu Yesu,**
**kwa kuwa hujitolea kikamilifu kwa kila mmoja wetu ukitualika kufanya vivyo hivyo.**
**Utukufu kwako, Roho Mtakatifu,**
**kwa maana hutukusanya kwa upendo na umoja.**
**Utukufu kwako, Mungu wa upendo,**
**kwako tumeumbwa, kuokolewa na kufanywa kitu kimoja. Amina.**

**Wimbo**

## Litania ya Sifa na Shukrani

M Hebu tuelekeze roho zetu kwa Mungu kwa sifa:

Sifa kwako Bwana kwa vile umemimina upendo wako rohoni mwetu ili kamwe tusife moyo. Unatuondolea uoga maishani mwetu kwa ajili ya upendo wako, na kutunza roho zetu zilizo jeruhiwa na kuumizwa. Twakusifu kwa ajili ya wanawake wote na wanaume wote wanaopanda mbegu za upendo na matumaini kwa jirani zao ulimwenguni kote.

**W Bwana tunakusifu.**

M Mungu wa milele, twakushukuru kwa zawadi ya Kristo mwanao, Mwokozi wa watu wote. Shukrani kwako kwa neema ya wongofu na mbegu zote za amani, matumaini na upendo miongoni mwa watu wako na kila pahali. Shukrani kwako kwa imani tuliopokea kutoka kwa mitume, kwa sala ya Yesu kwa umoja, na kwa zawadi ya Habari Njema ya wokovu.

**W Bwana, tunakushukuru.**

K Mungu wa upendo, tunakushukuru kwa ukarimu wa upendo wako kwa watu wote – Mungu wa upendo, tunakuabudu kwa ajili ya ukarimu wa upendo wako kwa watu wote – upendo kamili hata kupita fahamu yetu; upendo ambao haubagui kwa sababu za rangi, jinsia au hali ya jamii. Tunakuabudu uliyetutumia mwanao Yesu Kristo ulimwenguni kwa ajili ya upendo wako na unaendelea kumimina upendo huo maishani mwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu.

**W Bwana, tunakuabudu.**

## Sala ya kuungama

M Tunakuja mbele zako, ee Mungu, kuungama dhambi zetu:

W Kwa kutafuta furaha bila Mungu na kupuuza amri ya upendo, tumejitenga na Mungu na jirani yetu. Uchoyo wetu na tamaa ya kumiliki na kuthibiti imetutenganisha na Mungu.

*Kimya*

M Mungu wa rehema:
**W utusamehe na kutuponya.**

M Tunapokubali itikadi zinazodunisha utu wa wengine, tunajenga ukuta wa utengano, kupanda mbegu za chuki na vurugu na kuacha amri ya Bwana inayotaka tupendane.

*Kimya*

M Mungu wa rehema:
**W utusamehe na kutuponya.**

M Tumefanya roho zetu kuwa ngumu na kujidanganya. Kwa kutokuwa na huruma, tumeshindwa kumuona Kristo aliye ndani ya walio tofauti nasi.

*Kimya*

M Mungu wa rehema:
**W utusamehe na kutuponya.**

M Tumeshindwa kufungua roho na akili zetu kwa upendo wa Mungu kwa wote usio na kikomo na usio na masharti. Kwa kujitenga na upendo huu, ulimwengu unafunikwa na giza la uchoyo, vurugu, kutojali na kutoona maana [ya upendo].

*Kimya*

M Mungu wa rehema:

**W utusamehe na kutuponya.**

K Mungu, Baba wa Bwana yetu Yesu Kristo uliye mtuma tatika utimilifu wa wakati kuokoa viumbe vyote, tunakuomba uturehemu na kutubadilisha kwa Roho wako Mtakatifu.

**W Sifa kwa Mungu, tunaye msifu kwa sauti moja.**

## Mara tatu takatifu

**W Mtakatifu Mungu!**
**Mtakatifu mwenye nguvu!**
**Mtakatifu wa milele yote, utuhurumiye!**

## Somo kutoka Agano la Kale *Mwanzo 18 :1-8*

M Bwana akamtokea Ibrahimu karibu na mialoni ya Mamre, alipokuwa ameketi mlangoni pa hema yake mchana wakati wa hari.

[2] Akainua macho yake akaona, na tazama, watu watatu wamesimama mbele yake. Naye
alipowaona alipiga mbio kuwalaki kutoka mlangoni pa hema, akainama mpaka nchi,
[3] akasema, Bwana wangu, kama nimeona fadhili machoni pako nakuomba usinipite sasa mimi
mtumwa wako.

[4] Na yaletwe basi maji kidogo mkanawe miguu, mkapumzike chini ya mti huu.

[5] Nami nitaleta chakula kidogo, mkaburudishe moyo, baadaye mwendelee, iwapo mmemjia mtumwa wenu. Wakasema, Haya, fanya kama ulivyosema.

[6] Basi Ibrahimu akaenda hima hemani kwa Sara, akasema, Himiza vipimo vitatu vya unga safi, uukande, ufanye mikate.

[7] Ibrahimu akapiga mbio kwenda kundini, akaleta ndama wa ng'ombe aliye laini, mzuri, akampa mtumishi, naye akahimiza kuiandaa.

[8] Akatwaa siagi na maziwa, na ndama aliyoiandaa, akawaandikia mbele yao, akasimama karibu nao chini ya mti, nao wakala.

[9] Wakamwambia, Yu wapi Sara mkeo? Akasema, Yumo hemani.
[10] Akamwambia, Hakika nitakurudia wakati huu huu mwakani, na tazama, Sara mkeo atapata
mwana wa kiume. Sara akasikia mlangoni pa hema iliyokuwapo nyuma yake.
[11] Basi Ibrahimu na Sara walikuwa wazee, na umri wao mkubwa, na Sara alikuwa amekoma
katika desturi ya wanawake.

[12] Kwa hiyo Sara akacheka moyoni mwake, akisema, Niwapo mkongwe, nitapata furaha, na bwana wangu mzee?

[13] Bwana akamwambia Ibrahimu, Mbona Sara amecheka akisema, Mimi kweli nitazaa mwana, nami ni mzee?

[14] Kuna neno gani lililo gumu la kumshinda Bwana? Kwa muhula wake nitakurudia, wakati huu huu mwakani, na Sara atapata mwana wa kiume.

[15] Akakana Sara, akisema, Sikucheka, maana aliogopa. Naye akasema, Sivyo, umecheka.
[16] Kisha watu hao wakaondoka huko wakaelekeza nyuso zao Sodoma. Ibrahimu akaenda
pamoja nao awasindikize.

[17] Bwana akanena, Je! Nimfiche Ibrahimu jambo nilifanyalo,

[18] akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari, na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa? (WordProject, International Bible Association)

## Zaburi ya kuitikizana *Zaburi 138*

M Nitakusifu wewe, Ee BWANA, kwa moyo wangu wote, mbele ya "miungu" nitaimba sifa zako. Nitasujudu nikielekea Hekalu lako takatifu, nami nitalisifu jina lako kwa ajili ya upendo wako na uaminifu, kwa kuwa umelikuza jina lako na neno lako juu ya vitu vyote.

**W Nilipoita, ulinijibu.**

M Nilipoita, ulinijibu ; ulinifanya jasiri na mwenye moyo hodari ; Wafalme wote wa dunia wakusifu wewe Ee BWANA, wakati wanaposikia maneno ya kinywa chako.

**W Nilipoita, ulinijibu.**

M Wao na waimbe kuhusu njia za BWANA, kwa maana utukufu wa BWANA ni mkuu.
Ingawa BWANA yuko juu, humwangalia mnyonge, bali mwenye kiburi yeye anamjua kutokea mbali.

**W Nilipoita, ulinijibu.**

M Nijapopita katikati ya shida, wewe unayahifadhi maisha yangu, unanyoosha mkono wako dhidi ya hasira ya adui zangu, kwa mkono wako wa kuume unaniokoa. Bwana atatimiza kusudi lake kwangu, ee Bwana, upendo wako wadumu milele: usiziache kazi za mikono yako.

**W Nilipoita, ulinijibu.**

M Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu;

**A Kama mwanzo na sasa na siku zote, na milele. Amina.**

## Somo la Injili, *Luka 10:25-37*

M 25 Mwalimu mmoja wa sheria alisimama akajaribu kumpima Yesu, akamwuliza, “Mwalimu,
nifanye nini ili nipate uzima wa milele?” 26 Yesu akamjibu, “Sheria inasemaje? Unaitafsiri
vipi?” 27 Yule mwalimu wa sheria akajibu, “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa
nafsi yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote. Na umpende jirani yako kama
unavyojipenda mwenyewe.” 28 Yesu akamwambia, “Jibu lako ni sahihi. Fanya hivyo nawe
utaishi.” 29 Lakini yule mwalimu wa sheria akitaka kuonyesha kwamba hoja yake ilikuwa na maana
zaidi, akamwuliza Yesu, “Na jirani yangu ni nani?”
30 Yesu akamjibu, “Mtu mmoja aliteremka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko. Njiani akashambuliwa
na majambazi; wakamwibia kila kitu alichokuwa nacho, wakampiga wakamwacha karibu ya
kufa. 31 litokea kwamba kuhani mmoja alikuwa anapitia njia ile. Alipomwona huyo mtu, akapita
upande mwingine wa barabara akamwacha hapo hapo. 32 Vivyo hivyo Mlawi mmoja naye alipopita,
alimwona, akapita upande mwingine wa barabara akamwacha hapo hapo.
33 “Lakini Msamaria mmoja aliyekuwa akisafiri kupitia njia hiyo alipomkuta, alimwonea
huruma, 34 akamwendea akasafisha majeraha yake kwa divai na mafuta, akayafunga. Kisha akamweka
kwenye punda wake akaenda naye mpaka nyumba ya wageni ambapo alimtunza. 35 Kesho yake, yule
Msamaria alipokuwa anaondoka, akampa mwenye nyumba ya wageni fedha akamwomba amtunze
yule mgonjwa na akaahidi kulipa gharama yoyote ya ziada atakaporudi.
36 “Unadhani ni yupi kati ya hawa watatu alikuwa jirani yake yule mtu aliyeshambuliwa na
majambazi?”
37 Yule mwalimu wa sheria akajibu, “Ni yule aliyemwonea huruma.” Yesu akasema, “Nenda ukafanye
vivyo hivyo.” (Biblia Takatifu, SNT)

**Hymn**

## Sermon/Homily

*Followed by a moment of silence or a hymn.*

## Uthibitisho wa Upendo *imehamasishwa na Wakorintho 1:13*

*Nusu moja ya waumini wataimba mstari wa kwanza wa somo na wengine mstari wa pili.*

I Hata nikinena kwa lugha za binadamu na za malaika,
Kama sina upendo, nimekuwa kengele inayolialia au toazi livumalo.

II Ningekuwa na kipawa cha unabii na kujua siri zote na maarifa yote, na niwe na imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, mimi si kitu.

I Kama nikitoa mali yote niliyo nayo na kama nikijitolea mwili wangu uchomwe moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu.

II Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni wivu, hauna majivuno, hauna kiburi. Haukosi kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, haukasiriki upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya.

I Upendo haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli. Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini yote, hustahimili yote.
.

II Upendo hauna mwisho. Unabii? Utakoma. Lugha? Zitakoma.
Maarifa? Yatapita.

**W** **Imani, Tumaini na upendo itadumu.**
**Upendo ni bora kuliko yote.**

**Wimbo**
*Nafasi hii pia yaweza kutumika kutoa sadaka.*

## Maombi ya Maombezi

K Tuna alikwa kufuatia wito wa kumpenda Mungu na jirani kama nafsi yetu. Tunapokariri kujitolea kwetu kwa wito huu, twaomba upendo huu uimarishe umoja wetu wa Kikristo.

M Kwa mioyo yetu yote, twatamani kuishi katika upendo wake Mungu na kuwa na neema ya kupenda jirani zetu kama nafsi zetu.

Mungu wa upendo usio na mipaka, twaomba kwamba watu wote waweze kujua rehema yako isiyo kikomo na kuamini hamu yako ya kutujaza na upendo wako usio na mwisho.

**W** **Tujaze upendo wako! Tufanye kitu kimoja kwako.**

M Tunaomba pamoja na Kristo aliyeombea umoja wa wote wanao mfuata.

Mungu wa ushirika, tunaomba tufanye kazi pamoja kwa utukufu wako mkuu na kutangaza Habari Njema ya uokovu kwa wote.

**W** **Tujaze upendo wako! Tufanye kitu kimoja kwako.**

M Mioyo yetu imevunjika kwa ajili ya mkanganyiko na migawanyiko ulimwenguni.

Mungu mponyaji wetu, sisi tulio tawanyika kama kondoo wasio na mchungaji, kwakuomba utuutuweke pamoja. Tuchangamshe na Roho wako, na ututume tena wawili wawili kuwa mwanga wa ulimwengu na chumvi ya ardhi.

**W** **Tujaze upendo wako! Tufanye kitu kimoja kwako.**

M Ulimwengu wetu umejeruhiwa na ugaidi na vurugu. Mamilioni wanalazimika kuacha makwao kutafuta pahali pa kukimbilia na usalama.

Mungu wa makaribisho, tujalie neema ya kujihatarisha kwa niaba ya wageni, tukitunza vidonda vyao na kusimama pamoja nao. Imarisha azimio letu la kuwa wema na wa rehema na kutenda siku zote vile unavyo tutendea.

**W** **Tujaze upendo wako! Tufanye kitu kimoja kwako.**

M Kwa udhaifu wetu na umoja, twajua kwamba mara nyingi twapitia upande mwingine, tukiwahepa wanao hitaji usaidizi wetu.

Mungu mwenyezi, licha ya ukosefu wetu wa upendo, fungua mioyo yetu kutambua urefu, upana, na kina cha upendo wako, ili tuweze kukupenda zaidi na kupenda jirani zetu kama nafsi zetu.

**W** **Tujaze upendo wako! Tufanye kitu kimoja kwako.**

## Sala ya Bwana

K Kama watoto wa Mungu mmoja, tuombe vile Yesu alivyo tufunza:

**A** **Baba yetu uliye mbinguni, jina**
**lako litukuzwe, ufalme wako**
**ufike, utakalo lifanyike duniani**

**kama mbinguni. Utupe leo**
**mkate wetu wa kila siku.**
**Utusamehe dhambi zetu jinsi**
**tunavyo wasamehe walio**
**tukosea. Usitutie katika**
**kishawishi na utuokoe maovuni.**
**Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na**
**utukufu ni wako sasa na milele.**
**Amina.**

**Wimbo**

## Sala ya mwisho

**W** **Bwana Yesu, uliye omba kwamba tuwe kitu kimoja, twakuomba kwa umoja wa Wakristo wote, kulingana na mapenzi yako, na kulingana na uwezo wako.**
**Twaomba Roho wako atuwezeshe kuona mateso yanayoletwa na migawanyiko, kuona dhambi yetu na kutumaini bila kukata tamaa. Amina.**[7]

## Kutuma

*Kibuyu au chombo cha maji kinaletwa mbele na kuinuliwa mbele ya waumini, kiongozi akisema:*

K Tunapo changamshwa na maji ya uhai,
twendeni tumpende Mungu, na kupenda jirani zetu kama nafsi zetu,
pamoja na Kristo na kwa kuhuishwa na Roho Mtakatifu.

**W** **Chochote tunacho weza kufanya pamoja, hebu tufanye ! Amina!**

**Hymn**

# TAFAKARI ZA BIBLIA NA MAOMBI YA SIKU NANE

## SIKU YA 1

*Mwana sheria alisimama ili kumpima Yesu. "Mwalimu", alisema, "nifanyeje ili nirithi uzima wa milele?" (Luka 10:25)*

### Tusaidie, Bwana, ili tuwe na uhai ulio elekea kwako

**Masomo ya ziada**
Warumi 14:8-9
Zaburi 103:13-18

**Tafakari**
"Nifanye nini ili nirithi uzima wa milele?" Swali hili muhimu aliloulizwa Yesu na mwanasheria linamlenga kila amuaminiye Mungu. Linagusia maana ya uhai hapa duniani na milele. Kwingine katika Biblia, Yesu anatueleza maana kamili ya uzima wa milele: "… ili wakutambue, ewe Mungu wa kweli, na Yesu Kristo, uliyemtuma" (Yohana 17:3). Kumjua Mungu ina maana ya kugundua na kufanya mapenzi yake Mungu maishani mwetu. Kila mtu anatamani maisha kamili na ya ukweli, na Mungu pia, hutamani hivyo (cf. Yohana 10:10). Mtakatifu Irenaeus alisema, "Utukufu wa Mungu ni binadamu aliye hai kabisa".

Maisha yalio na migawanyiko, uchoyo na utesaji, mara nyingi hututenga na kumtafuta Mungu. Maisha ya Yesu yaonyesha siri ya maisha yaliyo karibu na Mungu Baba anayetamani kujaza watoto wake wote na uzima wa milele. Yesu ni "Njia" inayoelekea kwa Baba, hatima yetu ya mwisho.

Kwa hivyo, kutafuta kwetu kwa uhai wa milele hutuleta karibu na Yesu, na vilevile karibu na wenzetu, huku tukiimarisha ukaribu wetu kwenye njia ya umoja wa Kikristo. Na tukikaribisha urafiki na ushirikiano na Wakristo wa makanisa yote, tukiombea siku tutakapoweza kusimama wote pamoja mbele ya Meza ya Bwana.

**Sala**
Mungu wa uhai,
Umetuumba ili tuwe na uhai, uhai ulio kamili.
Na tutambue hamu ya maisha ya milele katika kaka zetu na dada zetu.
Tunapoamua kufuata njia ya Yesu, na tuongoze wengine kwako.
Tunaomba kwa jina lake. Amina.

## ***SIKU YA 2***

Mwanasheria alijibu, "*Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa nafsi yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote. Na umpende jirani yako kama nafsi yako.*"
*(Luka 10:27)*

# Bwana nisaidie nikupende, nimpende jirani yangu, na nijipende mwenyewe vile nilivyo

### Masomo ya ziada

Kumbukumbu ya Torati 10:12-13
Zaburi 133

### Tafakari

Jibu la mwanasheria laonekana sahili, kulingana na amri za Mungu zilizojulikana sana. Hata hivyo, mara nyingi ni vigumu kumpenda Mungu namna hiyo na jirani yetu vilevile.

Amri ya kumpenda Mungu yahitaji kujitolea kwa dhati na kujiachilia mbali kabisa, huku tukimtolea mioyo yetu na akili zetu kutenda utashi wake. Twaweza kuomba neema ya kufuata mfano wa Kristo, aliye jitolea kabisa akisema, "Sio mapenzi yangu bali yako utendeke." (Luka 22:42) Pia alionyesha upendo wake kwa wote, wakiwemo adui zake. Hatuchagui majirani zetu. Kuwapenda kuna maana ya kushughulikia mahitaji yao, kukubali kutokamilika kwao na kutia matumaini yao maanani. Mtazamo huo huo unahitajika kwa njia ya umoja wa Kikristo kuhusu tofauti za kimila.

Mwito wa kumpenda jirani kama "nafsi yako" watukumbusha umuhimu wa kujikubali tulivyo, tukifahamu macho ya Mungu ya Huruma kwetu, daima akiwa tayari kutusamehe. Zingatia kwamba u kiumbe anachokipenda Mungu. Jiheshimu. Kuwa na imani kwa nafsi yako. Vile vile, twaweza kuombea neema ya kupenda na kukubali kanisa letu au jumuiya yetu, licha ya upungufu wake, tukabidhi Baba yote, anayeturudisha tutakavyo kwa Roho Mtakatifu.

### Sala

Bwana, tujalie neema ya kukujua kwa undani
zaidi, ili tukupende kwa nafsi zetu zote.
Tujalie roho safi, tupende jirani zetu kama nafsi zetu.
Zawadi ya Roho Mtakatifu na ituwezeshe kukuona katika dada zetu na kaka zetu,
ili tupendane kwa upendo wako usio masharti. Kwa Kristo Bwana wetu. Amina.

## *SIKU YA TATU 3*

*"Nani jirani yangu?"*
*(Luka 10: 29)*

# Bwana, fungua mioyo yetu kwa wale tusio waona

### Masomo ya ziada

Warumi 13:8-10
Zaburi 119:57-63

### Tafakari

Mwalimu wa sheria alitaka kujihesabu haki, akitumaini kuwa jirani anayestahili kumpenda ni wa imani na ukoo wake. Hii ni silika ya binadamu. Tunapo alika watu nyumbani mwetu, mara nyingi ni wa hali moja nasi kijamii, kimtazamo kimaisha na kimaadili. Silika ya hutuelekeza kule tunakojua. Hii ni sawa na jumuiya zetu za kikanisa. Hata hivyo, Yesu anamwelekeza mwanasheria na wengine walio mzingira ndani zaidi katika mila zao, akiwakumbusha wajibu wao wa kukaribisha na kupenda watu wote bila kujali dini, mila na hali yao ya kijamii.

Injili yatufundisha kwamba kuwapenda wale tulio sawa nao silo jambo la ajabu. Yesu anatuelekeza kwenye maono makubwa kuhusu maana ya utu. Mfano huu waeleza kwa njia wazi anachokitaka Kristo kwetu – kufungua mioyo yetu zaidi na kutembea njiani mwake, tukipenda wenzetu jinsi yeye anavyo tupenda. Kwa kweli, Yesu anamjibu mwanasheria kwa kumuuliza swali lingine: si "nani jirani yangu", bali, "nani alithibitisha kuwa jirani wa aliyekuwa taabani?"

Nyakati za ukosefu wa usalama na uoga hutukabili wakati kutoaminiana na hali ya wasiwasi unaathiri uhusiano wetu. Hii ndio changamoto ya mfano huu leo: mimi jirani ya nani?

### Sala

Mungu wa upendo,
Unayeandika upendo mioyoni mwetu,
Tupe ujasiri wa kuona mbali na sisi
na kuona jirani katika walio tofauti nasi, ili tuwe wafuasi
kamili wa Yesu Kristo, aliye ndugu na rafiki yetu,
na aliye Bwana milele na milele. Amina.

## *SIKU YA 4*

*Alipomuona, alipita upande mwingine. (Lk 10:31)*

# Kamwe tusiwahepe walio mashakani

### Masomo ya ziada

Isaya 58:6-9a
Zaburi 34:15-22

### Tafakari

Huenda kuhani na Mlawi wanaopita upande mwingine walikuwa na sababu nzuri za kutosaidia: huenda walitarajiwa kutimiza mambo fulani ya kidini na kwa hivyo walikuwa kwa hatari ya kujitia najisi kama mjeruhiwa angalikuwa maiti. Lakini mara nyingi, Yesu aliukosoa uongozi wa kidini kwa kuweka kanuni mbele ya wajibu wa kutenda mema daima.

Utangulizi wa somo la Wiki ya Maombi waeleza jinsi Mwalimu wa sheria alivyotaka kujihesabia haki. Huenda kuhani na Mlawi katika mfano huu walijihesabu haki kwa kitendo chao. Kama Wakristo, tuko tayari kimo gani zaidi ya tunavyo tarajiwa? Wakati mwingine, mazoea yetu ya kuto ona mbali kutokana na kanisa na mila zetu kwaweza kutuzuia kuona kilicho wazi kutokana na maisha na ushuhuda wa dada na kaka zetu wa mila nyingine za Kikristo. Tunapo fungua macho kuona vile upendo wa Mungu anavyo onyeshwa na Wakristo wenzetu, tunasongeshwa karibu nao na hivyo kuingia katika uhusiano wa kindani nao.

Mfano wa Yesu hautupi tu changamoto la kutenda mema, bali pia kupanua uono wetu. Hatujifunzi tu kilicho kizuri na kitakatifu kutoka kwa wale tunao shiriki nao imani yetu au mtazamo wetu wa kidini, bali pia kutokana na wale tunao tofautiana nao. Mara nyingi, tusiye mtarajia ni Msamaria Mwema.

### Sala

Bwana Yesu Kristo,
Tunapotembea nawe katika safari ya umoja, macho yetu yasitazame kwingine, bali yawe wazi kwa ulimwengu. Tunaposafiri maishani,
Tusimame na kuwafikia, na kufunga vidonda vya walio athiriwa, na kwa kufanya hivyo, kuhisi kuwepo kwako ndani yao: unayeishi na kutawala milele na milele. Amina.

## *SIKU YA 5*

*Aliendda kwake na kumfunga vidonda, baada ya kuviweka mafuta na divai.*
*(Luka 10:34)*

# Bwana, tusaidie kuona vidonda na kupata tumaini

### Masomo ya ziada

Joeli 2:23-27
Zaburi 104:14-15, 27-30

### Tafakari

Msamaria Mwema alitenda alivyoweza kwa kutumia alichokuwa nacho: mvinyo na mafuta aliyoweka kwenye vidonda vya muathiriwa na kumweka kwa punda wake. Zaidi ya hayo, aliahidi kulipia matibabu ya muathiriwa. Tunapo ona ulimwengu kwa macho ya Msamaria, hali yoyote yaweza kuwa nafasi ya kumsaidia aliye mashakani. Hapa ndipo upendo unapojionyesha. Mfano wa Msamaria Mwema unatuhamasisha kujiuliza namna nunavyo jitolea kwa jirani aliye mashakani. Alipeana mvinyo na mafuta, huku akimuokoa na kumpa tumaini. Tutoe nini ili tujumuike na kazi ya Mungu ya kuponya ulimwengu ulio na majonzi?

Hali hii hujionyesha katika ukosefu wa usalama ulimwenguni, uoga, kutoaminiana na migawanyiko. Aibu ni kwamba migawanyiko hii iko hata miongoni mwa Wakristo. Ingawa twasherehekea sakramenti au ibada zingine za uponyaji, upatanisho na kufariji, mara nyingi tukitumia mafuta na divai, tunaendeleza migawanyiko inayo athiri Mwili wa Kristo. Uponyaji wa migawanyiko yetu ya Kikristo hukuza uponyaji wa mataifa.

### Sala

Mungu mwenye neema,
Wewe uliye chanzo cha upendo na wema wote:
tuwezeshe kuona mahitaji ya jirani zetu.
Tuonyeshe tunachoweza kufanya ili kuleta uponyaji.
Tubadilishe ili tuweze kuwapenda kaka na daza zetu.
Tuwezeshe kushinda vikwazo vya migawanyiko, ili tuweze
kujenga ulimwengu wa amani kwa wema wa pamoja.
Asante kwa kufanya viumbe vyako kuwa vipya na kutuelekeza siku za baadaye zenye matumaini:
wewe uliye Bwana wa wote, jana, leo na milele. Amina.

## *SIKU YA 6*

*Kisha aka muweka juu ya punda wake, akampeleka kwa nyumba ya wageni, na kumtunza. (Luka 10:34)*

# Bwana, geuza makanisa yetu yawe nyumba za wageni kukaribisha wenye mahitaji

### Masomo ya ziada

Mwazo 18:4-5
Zaburi 5:11-12

### Tafakari

Mtu aliyevamiwa na wanyang'anyi alitunzwa na Msamaria aliyeona zaidi ya ubaguzi na upendeleo. Msamaria aliona mtu aliyekuwa taabani akampeleka kwenye nyumba ya wageni. "Kesho yake, akatoa dinari mbili, akampa mwenye nyumba ya wageni, akasema: 'Mtunze, na nitakapo rudi, nitakupa malipo ya ziada utakayo kuwa umegharamia'" (Luka 10:35).

Katika jamii yoyote, ukarimu na ushikamano ni muhimu. Hii hujionyesha kwa kukaribisha wageni, wahamiaji na wasio na makao. Hata hivyo, pasipo usalama, shuku na vurugu, ni kawaida kutowaamini jirani zetu. Ukarimu ni ushuhuda muhimu wa Injili, hasa tunapozingatia dini na wingi wa kitamaduni. Kumkaribisha 'mwingine', nawe pia kukaribishwa, ni kiini cha mazungumzo ya kiekumene. Wakristo wana changamoto ya kubadilisha makanisa kuwa nyumba za wageni ambako jirani wanaweza kumpata Kristo. Ukarimu wa aina hiyo ni dalili ya upendo wa makanisa yetu kwa wao wenyewe na kwa watu wote.

Tunapo vuka mipaka ya imani zetu za kijadi na kuchagua ukarimu wa kiekumene, sisi kama Wakristo tunawacha kuwa wageni na kuwa majirani.

### Sala

Mungu wa upendo,
Katika Yesu, ulituonyesha maana ya ukarimu, kwa
kujali utu wetu ulio dhaifu.
Tufanye tuwe jamii inayo karibisha wanao jihisi kutelekezwa na kupotea
kwa kujenga nyumba ambamo wote
wanakaribishwa.
Na tukaribiane zaidi tunapo ukabidhi ulimwengu upendo wako usio masharti.
Tunaomba haya kwa umoja wa Roho Mtakatifu. Amina.

## *SIKU YA 7*

*Yesu akasema: "Kwa maoni yako, yupi kati ya hawa watatu alikuwa jirani?" (Luka 10:36)*

# Bwana, tuonyesha namna ya kushughulikia jirani yetu

### Masomo ya ziada

Wafilipi 2:1-5
Zaburi 10:17-18

### Tafakari

Alipomaliza kusimulia hadithi hii, Yesu alimwuliza mwanasheria: "Nani alikuwa jirani kwa mwathiriwa?" Mwanasheria alijibu "Yule aliye muonyesha huruma." Hasemi, "Msamaria" na yawezekana kuwa uhasama kati ya Wasamaria na Wayahudi ulifanya jibu kama hilo kuwa ngumu kukiri. Mara nyingi twakuta majirani pahali tusipotarajia kabisa, watu ambao hata kutamka majina yao au walipotoka ni ngumu kutamka. Katika ulimwengu wa sasa, ambapo siasa kali mara nyingi huleta ugomvi kati ya watu wa dini tofauti, Yesu anatupa changamoto kupitia mfano huu ili kutuonyesha umuhimu wa wito wetu wa kuvuka mipaka na kuta za utengano.

Sawa na mwanasheria, tuna changamoto ya kutafakari jinsi tunavyo ishi maisha yetu, sio tu kama tunatenda wema au la, lakini pia kama tunatelekeza huruma jinsi kuhani na Mlawi walivyofanya.

### Sala

Mtakatifu Mungu,
mwanao Yesu Kristo alikuja kwetu
kutuonyesha njia ya huruma.
Tuonyeshe kwa Roho wako mfano wa
kufuata ili kutimiza mahitaji ya watoto wako
wote, ili kutoa ushuhuda wa pamoja wa
Kikristo kuhusu njia zako za upendo na
Huruma.
Twaomba kwa jina la Yesu. Amina.

## *SIKU YA 8*

*Yesu alimwambia, "Nenda na ufanye vivyo hivyo" (Luka 10:37)*

# Bwana wetu, ushirika wetu na uwe ishara ya Ufalme wako

### Masomo ya ziada

Warumi 12:9-13
Zaburi 41:1-2

### Tafakari

Kwa maneno haya – "Nenda na ufanye vivyo hivyo" – Yesu anatutuma, na kila moja wapo ya makanisa yetu, kuishi kufuatana na amri wake wa upendo. Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, tunatumwa tuwe "Kristo wengine", tukiwaguza binadamu wanaoteseka kwa rehema na huruma. Kama Msamaria Mwema alivyo mtendea mwathiriwa, twaweza kuamua kutowakataa walio tofauti nasi na badala yake kudumisha desturi ya kuwa karibu na mapenzi mema.

Wito wa Yesu wa "Nenda na ufanye vivyo hivyo" wagusiaje maisha yangu? Wito huu wa Kristo una ashiria vipi uhusiano wangu na waumini wa makanisa mengine? Twawezaje kutoa ushuhuda wa pamoja kwa upendo wa Mungu? Kama mabalozi wa Kristo (linganisha na Wakorintho wa 2 Sura 5:20), tunaitwa kwa upatanisho na Mungu, kwa ushirika kutia mizizi na kukuwa katika makanisa yetu na pahali palipokumbwa na mizozo ya kijamii kama vile jimbo la Saheli.

Kadiri kuaminiana na kujiamini kunavyo ongezeka, itakuwa rahisi kwetu kukubali kuonyesha vidonda vyetu, vikiwemo vidonda vya kikanisa, ili upendo wa Kristo utuzuru na kutuponya kwa kupitia upendo na kujali kati yetu. Jitihada za pamoja kuleta umoja wa Kikristo unasaidia kujenga uhusiano upya, ili migogoro ipishe ushirika na upendo.

### Sala

Baba wa mbinguni,
tunakushukuru kwa kipaji cha Roho Mtakatifu, mwenye
kuleta uzima, anayetufanya kujifungulia wenzetu, anayetatua
mizozo, na kuimarisha umoja wetu.
Tufanye tukuwe kwa upendo na kutamani kutangaza neno la injili kwa uaminifu zaidi
ili ulimwengu uje pamoja kwa umoja
na kumkaribisha Mfalme wa
Amani. Kwa Kristo Bwana wetu.
Amina.

# KIAMBATISHO 1

## *Nyimbo zilizo pendekezwa wakati was Ibada**

### O JESUS PRINCE OF PEACE




1. O Jesus prince of peace,
my life and my beloved,
my saviour and my rock.
O Jesus, my strong tower,
my joy and strength you are,
Creation's morning star.

2. O Jesus, living Word
Bread broken for all people
And strength upon their way
O Jesus, flame of love
The broken spirit's rest
The Truth, the light of day.

3. O Jesus, risen Son
The hope of every nation
My one consoling friend
O Jesus, Master, King
My brother through your blood
My Saviour and my God.

Bm A D
G A D4 D
Em F# Bm
B Em A D
Em F# Bm
F# Bm


3. O Jesus, rising sun
On all our human suffering
My shepherd and my hope
O Jesus promised land
My treasure, my sole good
My maker and my Lord.

Original Title (FR) : Jésus prince de paix
Text and Music : Chemin Neuf Community
© 1992 Les Ateliers du Chemin Neuf
Desert Day, Friday, Hymn for Morning Prayer in Ordinary Time, Morning, Ordinary Time
SECLI : D621

*. These songs are proposed by the writing group from Burkina Faso which prepared the first draft of the Week of Prayer for Christian Unity 2024.

# We Praise You Lord

Words and music: Chemin Neuf Community




© Audiovisuel Musique Evangélisation AME - Réf. CD8-14
10 rue Henri IV, 69287 Lyon Cedex 02 - www.ame-boutique.com

# KIAMBATISHO 2

## *Sala kwa Umoja wa Wakristo*
## Inavyo ombwa na Jamii ya *Chemin Neuf*

*Ilivyo hamasishwa na sala ya Abbé Paul Couturier, Mwanzilishi wa Wiki ya Maombi ya Umoja ya Wakristo*

Bwana Yesu, uliyeomba kwamba tuwe kitu
kimoja, twakuomba ulete amani ya Wakristo,
kwa uwezo wa mapenzi yako na uwezo wako,
Roho wako na atuwezeshe kupata uzoefu wa mateso yanayotokana na migawanyiko,
kuona dhambi yetu, na kutumaini kupita kiasi.
Amina.

# KIAMBATISHO 3

## Sala ya Umoja wa Wakristo inavyo ombwa na Jamii ya *Chemin Neuf*

### Ishara ya kalisi[1] tupu na patena[2]

Kila siku, wanajumuiya ya *Chemin Neuf* husali, wakiomba Yesu, kupitia Roho Mtakatifu, "kutuwezesha kupitia mateso yanayoletwa na utengano".

Kueleza mfano huu, watu wawili wakifuatana wanabeba kalisi na patena tupu na kuziweka juu ya altare, kama ishara ya utengano wetu na dhambi ya kugawanyika. Wakati huo huo, wale wanaosali wanaombea "matumaini zaidi ya matumaini", wakiamini kuwa siku moja sote tutakusanyika mbele ya meza moja kuvunja mkate pamoja alivyosema Yesu – "fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi." (Luka 22:19)

### Wimbo wa Zaburi 122

*Kwa kawaida, wakati wa kuandamana kwenda altare na kalisi na pateni tupu, waumini huimba ZAburi 122, maneno yake yakimaanisha matembezi, hija hadi Yerusalemu, jiji takatifu, linalo ahidi umoja.*

**Nilifurahi walipo niambia**

(Kibwagizo hiki kwa kawaida huimbwa na madhehebu mbalimbali ya Kikristo wakati wa nyimbo za Sifa na Ibada. Waumini kufuata mwenye kuimba pekee).

[1] Kikombe kinachotumiwa kanisani kuwekewa mvinyo wakati wa ibada ya misa.
[2] Kisahani maalumu kinachotumiwa kanisani kuwekea Mkate Mtakatifu.

## *Utaratibu wa Ibada*

### Makaribisho na maonyesho

*Maelezo ya kalisi na pateni tupu, ikifuatiwa na Sala maalum ya Umoja wa Wakristo.*

### Kufungua

Ee Mungu, njoo utusaidie.
**Ee Bwana harakisha kutusaidia.**

**Atukuzwe Baba…**

### Zaburi 122 (Nilifurahi waliponiambia, "Twendeni nyumbani kwa Bwana!")

*Ikiimbwa, hali waumini wamesimama, na msafara wa kalisi na patena tupu ulielekea kuziweka juu ya altare.*

### Zaburi

*Zaburi moja au mbili au nyimbo, kuimbwa huku waumini wameketi, wakitangulia na kufunga na antifona.*

### Somo la Biblia

*Wote kuketi wakati wa somo. Mahubiri yaweza kufuata somo, ushuhuda, onyesho kuhusu kanisa la kiekumene au somo kutoka kwa mwandishi wa Kikristo.*

### Wimbo wa Zekaria (Luka 1:68-79)

*Huimbwa, huku waumini wamesimama, wakiimba antifona kabla na mwisho wa wimbo wa Zekaria.*

### Sala za maombezi

*Zikiwemo dua (au shukrani au baraka) kwa makanisa yetu, viongozi wao au kichezo maalum.*

### Sala kwa Umoja wa Makanisa

*Tazama hapo juu, kiambatisho 2.*

### Sala ya Baba yetu

### Sala ya Mwisho

### Mwisho

Tumbariki Mungu.
**Asante kwa Mungu.**

**Harakati za Kiekumene za Kimataifa -Sura ya Kenya (IEM-K)**

*Kijitabu hiki kimekusanywa na Jumuiya ya Kimataifa ya Kiekumene-Sura ya Kenya (IEM-K), kutoka kwa maandishi yaliyoandaliwa na Kamati iliyopewa mamlaka hayo kwa makubaliano ya pamoja ya Baraza la Kipapa la Kukuza Umoja wa Kikristo PCPCU) na Tume ya Imani na Utaratibu ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni. (WCC).*

*IEM-K ni shirika hiari la uanachama kule mashinani katika huduma ya kiekumene nchini Kenya. Washiriki wa harakati ya kiekumene, Kenya, hukutana kwa maombi ya ushirika kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi, mikutano miwili ya Meza Duara kila mwaka ili kujadiliana juu ya maswala yaliyoko na mada zinazoibuka, halafu pia tunakuwa na Mkutano wa Kitaifa wa Kiekumene kila baada ya miaka mitatu (Tarehe ya mkutano ujao itatangazwa).*

*Harakati ya IEM-K hushirikiana na makanisa, mashirika, na taasisi zinazojitolea kwa umoja ili kupanga na kutekeleza juhudi za kiekumene katika muktadha wetu. Daima iko tayari kulisaidia kanisa lolote, shirika au taasisi katika elimu ya kiekumene na maendeleo.*

**MAWASILIANO:** Barua pepe: info@iemkenya.org

http://www.iemkenya.org/